




# JIMBO KUU KATOLIKI LA DAR ES SALAAM

**PAROKIA YA KUNG'ARA KWA YESU KRISTO, MBEZI MSHIKAMANO**

S.L.P. 280 D'SALAAM, +255 686 794177, E: katolikimshikamano@gmail.com


## MATANGAZO: DOMINIKA 31 YA MWAKA – KUMBUKUMBU YA WAAMINI MAREHEMU WOTE - 02.11.2025

| | | |
|---|---|---|
| 1. | LEO DOMINIKA 02.11.2025 | **KUMBUKUMBU, KUWAOMBEA WAAMINI MAREHEMU WOTE**<br>Mchango wa pili kwa ajili ya ujenzi. |
| 2. | JUMATATU 03.11.2025 | Kumbukumbu ya Mt. Martin wa Pores |
| 3. | JUMATANO 05.11.2025 | Kumbukumbu ya Wat. Zakaria na Elizabeth, wazazi wa Mt. Yohane Mbatizaji |
| 4. | JUMAMOSI 08.11.2025 | Kutakuwa na Misa ya kuhitimisha matembezi ya Sanamu ya Bikira Maria katika **Kanda H** saa 1:00 asubuhi na kukabidhi Sanamu kwa **Kanda I**. Jumuiya zihimize na kufuatilia bahasha za Kapu la Mama na kuzirejesha katika Misa za kuhitimisha matembezi ya sanamu. Kutegemeana na hali, Misa ya hitimisho la matembezi **Kanda G** na kukabidhi **Kanda H** itafanyika siku moja katikati ya wiki jioni. |
| 5. | JUMAMOSI 08.11.2025 | Utafanyika uchaguzi wa Kamati Tendaji za Kanda zote Jumamosi ijayo 08.11.2025 saa 12:30 asubuhi. Kanda zipange mahali pa kusali na kufanya uchaguzi. Wahusika ni viongozi wa Kamati Tendaji za Jumuiya za Kanda husika na Wenyeviti wa Vyama vya Kitume wa Kanda na Kamati Tendaji ya Kanda inayomaliza muda wake. |
| 6. | DOMINIKA 09.11.2025<br><br>MISA MOJA TU – HITIMISHO LA MAVUNO | **DOMINIKA YA 32 YA MWAKA C**<br><br>**Misa ya 1: Saa 1:30 asubuhi**<br>Wasimamizi: Jumuiya ya Kung'ara kwa Yesu Kristo na Mt. Brigita wa Sweden<br>Watangaza Neno: Fredy Dominick na Ivon Dominick<br>Mchango wa pili ni kwa ajili ya ujenzi. |
| 7. | UCHAGUZI WA VIONGOZI VYAMA VYA KITUME KANDA | Kanda zilizofanya chaguzi za Vyama vya Kitume zinatakiwa kuwasilisha fomu za matokeo, na chaguzi zilizobakia viongozi wa Kanda watafute utaratibu wa kukamilisha kabla ya uchaguzi wa Kamati Tendaji za Kanda Jumamosi ijayo. |
| 8. | HITIMISHO LA MAVUNO PAROKIA 2025 | Hatujaweza kuhitimisha Mavuno Parokia leo 02.11.2025 kutokana na changamoto zilizojitokeza kipindi cha uchaguzi mkuu pamoja mitandao ya fedha kutofanya kazi, tunaalikwa kuendelea kukamilisha ahadi zetu na viongozi wa Jumuiya wafuatilie na kutoa taarifa. Hitimisho sasa litafanyika Dominika ijayo 09.11.2025. |

| | | |
|---|---|---|
| 9. | UCHAGUZI WA UTOTO MTAKATIFU | Kila Jumuiya inatakiwa kuchagua na kuwasilisha majina ya walezi wawili wa Utoto Mtakatifu (mwanamume na mwanamke) ifikapo Dominika ijayo, na uchaguzi wa viongozi wa Utoto Mtakatifu utafanyika kwa Jumuiya zote 15.11.2025. Viongozi wa Utoto wanakuwa 6 ikiwepo nafasi ya Mtunzahazina Msaidizi. |
| 10. | BAHASHA ZA MFUKO WA UINJILISHAJI - PAPA | Tumepokea bahasha za Marafiki wa Mashirika ya Uinjilishaji ya Baba Mtakatifu (PMS), kila Jumuiya itagawiwa kati ya Bahasa 2 au 3 leo na wanaombwa kuchangia kwa ukarimu. Kurejesha tarehe 30.11.2025. |
| 11. | VITI VYA PAROKIA | Jumuiya zilizoomba kununua viti zikamilishe taratibu za malipo ili Parokia inunue viti vingine wiki ijayo. |
| 12. | KUWAOMBEA MAREHEMU | Mwezi Novemba ni mwezi wa kuwakumbuka na kuwaombea marehemu wetu. Fomu za kuwaombea zimetolewa na tutatakiwa kuweka sadaka ya nia ya kuwaombea katika Misa. Fomu na sadaka ziwekwe kwenye bahasha na kufungwa.<br><br>Jumamosi ya 15.11.2025, tutafanya usafi katika makaburi ya Kibaoni mara baada ya Jumuiya, saa 2:00 asubuhi. |
| 13. | HUDUMA YA AFYA NA USHAURI WA SHERIA | Kutakuwa na huduma ya kupima afya na ushauri, pamoja na ushauri wa kisheria hapa Parokiani Dominika ya 16.11.2025 kupitia wataalamu wetu wa Parokia bila gharama kwa waamini. Huduma itaanza kutolewa mara baada ya Misa ya kwanza.<br><br>**Kupima afya:** uzito, urefu, sukari, shinikizo la damu, saratani ya shingo ya kiazi na ushauri.<br><br>**Ushauri wa sheria:** changamoto za majina kwenye vitambulisho na vyeti, kupiga mihuri nakala za vyeti, ushauri mwingine wa kisheria. |
| 14. | MAREJESHO YA VITABU | Jumuiya zinakumbushwa kufanya malipo ya vitabu vya Liturujia ya Sikukuu ya sikukuu ya Parokia tarehe 10.08.2025. |
| 15. | WARSHA YA WAAMINI WOTE JIMBO | Warsha ya waamini wote wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam itafanyika Jumamosi 29.11.2025 katika viwanja vya Parokia ya Kristo Mfalme Tabata kuanzia saa 2:00 asubuhi. Kutakuwa na Mada mbili,<br>1. Uchaguzi/Uongozi katika Kanisa 2. Mwaka wa Jubilei Kuu<br>Kutakuwa pia na vyeti kwa wenye Jubilei za miaka 25, 50 na 75.<br>**Sasa ada ya ushiriki imeondolewa, ushiriki ni bure, tujiandikishe kwa wingi. Watakaoshiriki watachangia nauli sh. 5,000/=.**<br>***Kila Jumuiya inatakiwa kuwasilisha taarifa ya maendeleo ya uandikishaji washiriki wa Warsha kwani inatakiwa Jimboni.*** |
| 16. | GAZETI LA TUMAINI LETU | Viongozi wa Jumuiya wanakumbushwa kuchukua Gazeti la Tumaini Letu ofisini na kufanya malipo ya nakala 4 kati ya 5. |

***Kauli Mbiu ya Mwaka wa Jubilei Kuu: "Jubilei 2025 – Mahujaji wa Matumaini."***

## MATEMBEZI YA SANAMU YA BIKIRA MARIA KATIKA MWEZI WA ROZARI NA KAMPENI YA KAPU LA MAMA MARIA 2025

| WIKI | TAREHE | KANDA HUSIKA | MSA YA HITIMISHO |
|---|---|---|---|
| 1 | 28/09 - 04/10 | A | SAA 1:00 ASUB |
| 2 | 04/10 – 11/10 | B | SAA 1:00 ASUB |
| 3 | 11/10 – 18/10 | C | SAA 1:00 ASUB |
| 4 | 18/10 – 25/10 | D & E | SAA 1:00 ASUB |
| 5 | 25/10 – 01/11 | F & G | SAA 1:00 ASUB |
| 6 | 01/11 – 08/11 | H | SAA 1:00 ASUB |
| 7 | 08/11 – 15/11 | I | SAA 1:00 ASUB |
| 8 | 15/11 – 22/11 | J | SAA 10:00 JIONI |
| 9 | 22/11 – 29/11 | K | SAA 10:00 JIONI |

## MATANGAZO NDOA KWA MARA YA TATU

1. Frank Samwel Mruma BIN Samwel Simon Mruma na Maria Rajabu Mchomvu wa Parokia ya Mbezi Mshikamano

   Anatarajia kufunga ndoa na:

   Lightness Anold Mariki BINTI Anold Yohane Mariki na Kristina Makyao wa Parokia ya Mbezi Mshikamano

2. Nobert Alfons Matage BIN Alfons Matage na Theodosia Mbanga wa Parokia ya Mbezi Mshikamano

   Anatarajia kufunga ndoa na:

   Anna Raphael Mngazija BINTI Raphael Mngazija na Aisha (Suzana) Ramadhani wa Parokia ya Mbezi Mshikamano

## MASOMO DOMINIKA – DOMINIKA YA 32 YA MWAKA C - 09.11.2025 (KUTABARUKIWA BASILIKA LA LATERANI)

| | |
|---|---|
| SOMO I | 2 Mak 7:1-2, 9-14 |
| WIMBO WA KATIKATI | Zab 17:1, 5-6, 8, 15 (K)15 |
| SOMO II | 2The 2:16-3:1-5 |
| SHANGILIO | Yn 1:12, 14 |
| INJILI | Lk 20:27-38 |